Dodoma, Agosti 19, 2026

# KUSITISHWA KWA LESENI YA GAZETI LA MWANAHALISI KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (6)

Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO) inapenda kuujulisha Umma kuwa leseni ya gazeti la MwanaHALISI imesitishwa kwa miezi sita (6) kuanzia tarehe 19 Agosti, 2026 kutokana na kukiuka sharti la 3 katika Leseni ya machapisho linalovitaka vyombo vya habari kuzingatia Sheria ya Huduma za Habari (Sura 229) na Kanuni zake (2017).

Gazeti hili lilitenda kosa hilo kwa kuchapisha kwenye kurasa ya 1, 2, na 3 katika toleo namba 571 la tarehe 6 - 12 Agosti, 2026, maudhui yaliyobebwa na kichwa cha habari kilichosomeka **“Nchimbi agoma kujiuzulu”** pasipo kutimiza wajibu wa kuzingatia usahihi na mizania kabla ya kuchapisha na kusambaza habari kwa umma. Aidha, hatua hii inachukuliwa kutokana na gazeti hili kuwa na mwenendo wa kurudia makosa yaliyokwisha kuonywa ambapo kumbu-kumbu zinaonesha kuwa mnamo tarehe 8 Mei, 2026, gazeti hili lilipewa onyo la maandishi baada ya makosa haya haya kutendeka katika toleo namba 557 la Aprili 30 hadi Mei 6, 2026. Taaluma ya uandishi wa habari ni taaluma adhimu na inayohitaji kutumiwa kwa umakini na uangalifu wa hali ya juu ili kuepusha upotoshaji na kuhakikisha jamii inapata habari sahihi, za ukweli na ambazo kutafutwa, kuchakatwa na kuchapishwa kwake kumezingatia Sheria, Kanuni,weledi na misingi ya taaluma ya uandishi wa habari inayotumika kote duniani.

Kwa muktadha huo, Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), alipoona kuwa gazeti hili limetenda kosa la kukiuka masharti ya Leseni iliyotolewa na Idara chini ya Sheria (Sura 229) pamoja na Kanuni zake (2017) kama zilivyorekebishwa mwaka 2024 na kwamba ikithibitika linaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria, alitoa fursa kwa gazeti hili kufika Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO), kwa ajili ya kusikilizwa juu ya makosa tajwa, kikao kilifanyika katika ofisi ndogo ya Dar es salaam siku ya tarehe 7 Agosti, 2026.

Baada ya majadiliano ya kina gazeti lilipewa fursa nyingine ya siku tatu kuwasilisha maelezo ya ufafanuzi kwa maandishi kumwezesha Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), kuelewa mazingira yaliyopelekea makosa hayo kutendeka.

Maelezo husika yalipowasilishwa Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO), ilibainika kuwa ufafanuzi uliyotolewa haukidhi haja ya kuliondolea gazeti hili wajibu wa kuzingatia misingi hiyo ya kitaaluma, hususan ikizingatiwa kuwa gazeti hili ni kongwe na lina waandishi pamoja na wahariri wenye uzoefu wa muda mrefu katika tasnia ya habari. Wakati wa majadiliano na katika maelezo ya maandishi ya gazeti hili zilibainika dosari kadhaa dhidi ya misingi ya kiuandishi ikiwemo kukosekana kwa usahihi na umakini katika kuhariri habari. Dosari hii ilithibitika baada ya kuonekana kuwa katika ukurasa wa pili wa gazeti hili kumetumika picha ya Mhe. Paul Christian Makonda, ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo na chini ya picha hiyo kuna maelezo yanayomtaja kuwa ni Mhe. Balozi, Dk. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hii ni dosari ya mwandishi pamoja na mnyororo mzima wa wahariri unaohusika katika kuhakiki usahihi wa taarifa zilizoandikwa kabla ya hatua ya kuchapisha gazeti husika.

Dosari nyingine ilikuwa ni kukosekana kwa mizania ya habari. Hii ilithibitika katika habari husika kutokana na mwandishi kutochapisha maelezo ya upande wa pili wa habari. Maelezo ya habari hii yanajikita katika kuzungumzia kujiuzulu kwa Mhe. Balozi, Dk. Emmanuel Nchimbi, lakini hayaoneshi mahala popote ambapo Mhe. Dk. Emmanuel Nchimbi, mwenyewe amehojiwa na kusema lolote juu ya suala hilo. Aidha, habari hii imeandika juu ya hoja zinazodaiwa kutolewa na Mhe. Paul Makonda, tena kwa kumnukuu, lakini hakuna mahali ambapo Mhe. Paul Makonda amenukuliwa kuthibitisha au kuonesha yeye ndiye aliyesema hoja hizo.

Dosari nyingine iliyothibitika ni kutokuweka uthibitisho wa taarifa alizochapisha. Katika habari husika mwandishi hajaonesha mahali popote alipochukua jitihada za kuwahoji hata mmoja wa viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) au watu waliokuwa wajumbe wa kikao hicho, mathalani, Katibu Mkuu, Katibu Mwenezi au Afisa Habari wa Chama cha Mapinduzi (ccm), ili kuthibitisha hayo yanayodaiwa kuwa yalijadiliwa katika kikao hicho, baada ya kuwa ameambiwa na vyanzo fiche.

Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), pia amezingatia mwenendo wa gazeti hili kurudia makosa haya licha ya kuwa makosa hayo yalishaonywa huko nyuma, mathalani, tarehe 17 Februari, 2026, gazeti hili liliandikiwa barua yenye kumbukumbu. na. IH/PML/RD/357/13, kuwataka wawasilishe maelezo ya maandishi kutokana na gazeti la tarehe 12-18 Februari, 2026, kuandika habari iliyokuwa na kichwa cha habari kilichosema **“Samia wa 2021 atakutana lini na wa 2026?”** ambalo lilimwelezea, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa ni dikteta. Tarehe 18 Februari, 2026, waliwasilisha maelezo husika kwa barua yenye kumbukumbu na. HHPL/ADM/ 05/04 na baada ya kusoma maelezo hayo Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO), iliwaita wahariri ofisini na kufanya nao kikao ambacho kiliisha kwa Idara hiyo kutoa onyo la mdomo.

Mnamo tarehe 1 Mei, 2026, gazeti hili liliandikiwa wito wa kuhudhuria kikao kutokana na kuchapisha maudhui hasi katika toleo na. 557 la tarehe 30 Aprili - 6 Mei, 2026, lililokuwa na vichwa visemavyo **“ICC haikwepeki”**, **“Hawa kuchongewa”** na **“Watang’oka tu”** ambavyo vilibainika kuwa na maudhui potofu na yasiyo zingatia sheria, misingi na maadili ya taaluma ya uandishi wa habari ikiwa ni pamoja na kutumia picha ya mtu mwingine katika wadhifa wa Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa (DGIS).

Tarehe 07 Mei, 2026, gazeti liliitwa katika kikao na lilitoa maelezo ya ana kwa ana na baadaye kupewa nafasi nyingine kupitia barua yenye Kumb. na.IH/PML/RD/357/16 ya tarehe 06/05/2026 kujitetea kwa maandishi ‘kwanini wasichukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria’. Walipowasilisha utetezi wa maandishi kwa barua yenye Kumb. Na. HHPL/ADM//05/13 ya tarehe 07 Mei, 2026, Idara kupitia barua yenye Kumb Na. IH/PML/RD/357/17 ya tarehe 08/05/2026 ilitoa onyo la maandishi kwa gazeti na kuwataka wahariri wa gazeti hili kuimarisha weledi katika uhariri wa maudhui na kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa inazozichapisha kabla ya kusambaza gazeti kwa umma. Barua hiyo ya onyo ilibainisha kuwa endapo ukiukaji huo utajirudia, Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO), haitasita kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.

Kwakuwa dosari ambazo zilizobainika katika habari husika zimejirudia kutoka katika dosari zilizosababisha gazeti hili kupewa onyo la maandishi tarehe 08 Mei, 2026, na kwakuwa makosa haya yametendeka miezi mitatu (3) tu baada ya makosa kama hayo kuonywa kwa maandishi, Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), amejiridhisha kuwa ni vema gazeti hili lipewe adhabu inayozidi ile iliyotolewa awali.

Kwa mantiki hiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), ametumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 9(b) cha Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229, kuamua kusitisha leseni ya kuchapisha na kusambaza gazeti la MwanaHALISI kwa kipindi cha miezi sita (6), kuanzia tarehe 19 Agosti, 2026. Aidha, kwa kuzingatia tafsiri ya neno "Newspaper" katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Huduma za Habari, uamuzi huo unahusu pia uzalishaji na usambazaji wa gazeti hilo kwa njia ya kielektroniki au mtandao kwa kipindi chote ambacho leseni husika imesitishwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229, gazeti hili linayo haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwa Waziri mwenye dhamana ya habari ndani ya siku thelathini (30) tangu tarehe ya uamuzi kutolewa.

**Wakati huo huo**, Mkurugenzi Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO), ameliandikia gazeti la Jamvi la Habari kulitaka lifike katika kikao na kuwasilisha maelezo kwa maandishi juu ya kwa nini lisichukuliwe hatua stahiki za kisheria kutokana na gazeti hilo kupitia matoleo kadhaa ya hivi karibuni yakiwemo Toleo Na.2985 la tarehe 15 Agosti, 2026 na Toleo Na. 2987 la tarehe 17 Agosti, 2026 kuchapisha maudhui ambayo kimantiki hayazingatii ipasavyo wajibu wa chombo cha habari ulioainishwa katika vifungu vya 7(2)(a)(iii) na 7(3)(b) na (e) vya Sheria tajwa na kanuni za 5(1)(a),(f)na(I), 5(3) na 5(4).

Aidha, gazeti hili pia limekuwa likikiuka Kanuni ya 6(1) ambayo inatoa wajibu wakuwasilisha nakala za machapisho yake kila yanapotolewa kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO). Gazeti hili kama ilivyo kwa magazeti yote yanayosajiliwa chini ya Sheria yana wajibu wa kuwasilisha nakala mbili za gazeti linalosambazwa kwa njia ya kawaida na nakala ya gazeti la kielektroniki lililosambazwa kwa njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Huduma za Habari (MAELEZO), anatoa wito kwa wamiliki wote wa vyombo vya habari kuzingatia Sheria ya Huduma za Habari, Sura namba 229 ya mwaka 2016 na anatoa onyo kwa wote ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wakikiuka wajibu wa kutekeleza Sheria hii.

**Imetolewa na**
**Idara ya Huduma za Habari (MAELEZO)**